**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

NAMBA ZA SIMU

MKUU WA SHULE: 0680106842/0620685407

MAKAMU MKUU WA SHULE: O788386580

SHULE YA SEKONDARI KYERWA MODERN,

S.L.P123,

KYERWA.

Tarehe …………

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi...........................................................................**
**S.L.P …..........................**
**...........................………………………….**

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KYERWA MODERN HALMASHAURI YA KYERWA MKOA KAGERA MWAKA …………..**

Ninayo furaha kukutarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha tano (v) mchepuo wa EGM kwa mwaka wa masomo …………. mhura wa masomo kwa kidato cha tano (v) utaanza tarehe ………….. na wewe mwanafunzi utatakiwa kufika shuleni tarehe …………..

MAHALI SHULE ILIPO

- Shule ya sekondari KYERWA MODERN ni ya serikali .Shule hii iko mkoani KAGERA wilaya ya KYERWA na ipo kyerwa mjini upande wa kusini magharibi mwa jengo la halmashauri.Shule ipo kilomita 1 (moja) kutoka jengo la halmashauri na ni mwendo wa dakika kumi na tano kwa miguu.

MAAGIZO

1.1 WAVULANA (SARE)

Suruali tatu (03)

i) Mbili rangi ya kijivu (Gray) kitambaa Kizito

ii) Moja rangi ya maroon iliyokaza kwa ajiri ya shamba dress

NB: Utatakiwa uje na suruali zote tatu zilizoshonwa vizuri na zenye mifuko mitatu, marinda (celebrations) na pana miguuni isiyopungua inchi kumi na saba (17) hatutahitaji suruali zilizoshonwa mtindo wa jeans.

- Mwanafunzi aje na shati mbili (2) rangi nyeupe mikono mirefu.
- Viatu vyeusi vya Kamba visivyo na visigino virefu soksi ndefu pea tatu nyeusi
- Sweta rangi ya darkblue shingo yake iwe na umbo la v.
- Alete ndoo ndogo mbili (2) za plastiki ya lita 10 rangi ya blue
- Aje na Godoro futi 21/2 (mbili na nusu) kwa sita (6)
- Aje na shuka jozi mbili (2) moja rangi ya pinki na moja rangi ya blue bahari.
- Aje na blanketi zito la kutosha kujisitili kipindi cha baridi.
- Aje na mto mkubwa wa kulalia mmoja na foronya mbili (2)
- Aje na mswaki , dawa ya meno, sabuni za kutosha na kandambili jozi moja (1) rangi ya blue.
- Aje na T-shirt ya rangi ya damu ya mzee (maroon) yenye kola.
- Aje na ream mbili (4) ya karatasi A4 kwa mwaka (ream mbili kwa kila muhula)
- Aje na bima ya afya (Hii ni muhimu sana) -
- Nguo za nyumbani haziruhusiwi
- Aje na Tai rangi ya kijivu iliyokaza isiyo na michirizi
- Aje na chandarua kujikinga na mbuu.
- Aje na taulo moja.

1.2. <u>WASICHANA (SARE):S</u>

- Mwanafunzi aje na sketi mbili (2)
    i. Rangi ya kijivu iliyokaza (Gray) (Kijivu nyeusi)

\- **<u>Ushonaji</u>**: Linda moja kubwa yaani katikati, mbele na nyuma , marinda mawili madogo mkono wa kulia na kushoto baada ya lindabox, upana wa marinda ni nchi mbili (knife edge pleats) upana wa mkanda usiozidi inchi mbili. Sketi iwe na urefu wa kutosha (juu ya kisigino ) kiwe kitambaa Kizito.

    ii. Aje na gauni mbili (2) za rangi ya blue bahari kwa ajiri ya shamba dress ndefu inchi kumi chini ya magoti.

- Aje na shati (2) nyeupe zenye mikono mirefu
- Aje na viatu vyeusi vya Kamba visivyo na visigino virefu.
- Soksi nyeupe ndefu jozi tatu (3) (stockings)
- Sweta rangi ya darkblue shingo yake iwe na umbo la V
- Alete ndoo ndogo mbili (2) za plastiki ya lita 10 rangi ya blue
- Rangi ya Hijab (juba) ni nyeupe kwa waislamu na kitambaa ndani ya juba kiwe cheupe na awe na zaidi ya moja.
- Aje na Godoro futi 2.5 mbili na nusu kwa sita.
- Aje na shuka 2 (mbili) moja rangi ya pinki na moja rangi ya blue bahari
- Aje na blanketi zito la kutosha kujisitili kipindi cha baridi
- Aje na taulo moja.

- Aje na mswaki, dawa ya meno, sabuni za kutosha na kandambili jozi moja (1) rangi ya blue.
- Aje na mto mkubwa mmoja (1) na foronya mbili (2)
- Aje na chandarua kujikinga na mbu.
- Aje na T-shirt ya rangi ya damu ya mzee (maroon) yenye kola.
- Aje na ream mbili (4) ya karatasi A4 kwa mwaka (ream mbili kwa kila muhula)
- Nguo za nyumbani haziruhusiwi
- Aje na bima ya Afya (Hii ni muhimu sana)
- Aje na Tai rangi ya kijivu nyeusi  isiyo na michirizi

NB: Mwanafunzi anapokwenda kuabudu (kanisani/msikitini) atatakiwa kuvaa sare za shule kama kawaida na si vinginenevyo.

1.3 <u>VIFAA VYA MICHEZO</u>.

WAVULANA:

a) Bukta moja 1 na Tracksuti ya rangi nyeusi yenye michirizi myeupe pembeni.
b) Raba jozi moja (1) (Au viatu vya michezo)
c) Fulana (T-shirt) blue bahari yenye mikono mifupi
d) Soksi jozi moja (1) ziwe ndefu rangi ya njano.

WASICHANA

a) Bukta moja (1) na Track- suti moja rangi nyeusi yenye michirizi myeupe pembeni.
b) Raba jozi moja (1)
c) Fulana (T- shirt) blue bahari yenye mikono mifupi.
d) Soksi jozi moja (1) ziwe ndefu rangi ya njano.

1.4. VIFAA VYA USAFI.

Kila mwanafunzi aje na

i. Jembe lenye mpini 01
ii. Blash ngumu (hard broom) 01
iii. Blash laini (soft broom) 01
iv. Mopa 01
v. Fyekeo/ kwanja 01
vi. Toilet paper 06 kila muhula (12 kwa mwaka)
vii. Reki 01
viii. Mfagio mmoja wa nje
ix. Sabuni ya maji lita 5 (2 kwa mwaka)

1.5 <u>VIFAA VYA CHAKULA</u>

- Huduma ya chakula itakuwepo, wanafunzi watapata uji chakula cha mchana na jioni unapokuja uje na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya chakula
  I. Sahani
  II. Kikombe rangi ya blue bahari
  III. Bakuli rangi ya blue bahari
  IV. Kijiko
  V. Kifaa cha kutunzia maji ya kunywa

2. MICHANGO MBALIMBALI

| NA | AINA YA MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

- Malipo haya yalipwe kwenye akaunti ya shule namba 0150770173300 (CRDB) Benki jina la akaunti KYERWA MODERN SECONDARY SCHOOL.
- Mwanafunzi atatakiwa alete "pay in slip" shuleni baada ya kutoa nakala (photocopy) **(mwanafunzi aje na vifaa vyote na sio pesa)**

2.2 <u>VIFAA VYA MASOMO</u>

- Unatakiwa kuja / kuleta vifaa vya masomo kama ifuatavyo
    - Madaftari makubwa (Counter books) saba (7) 4 quires kwa ajiri ya masomo yote atakayosoma.
    - Kalamu za wino mweusi na bluu na za risasi
    - Mkebe wa Hisabati (mathematical set)
    - Ni muhimu kila mwanafunzi kuja / kununua vitabu vya masomo atakayosoma kwa tahasusi husika
    - Anunue scientific calculator (shuleni pia zinapatikana (Tsh 30,000/=) tu
    - Mwanafunzi wa mchepuo wa sayansi anatakiwa kuja na koti jeupe kwa ajiri ya kuvaa anavoingia maabara kujifunza kwa vitendo, (Practical studies)

2.3 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

I. Mwanafunzi apimwe na daktari Hospitali ya serikali. Tumia fomu ilioyoambatanishwa.
II. Kusoma na kuzielewa sheria / kanuni za shule.
III. Kuwa na bima ya Afya.
IV. Kujaza fomu ya maelekezo yanayo husika (taarifa binafsi)
V. Kila mwanafunzi anatakiwa kuleta picha nne (4) za wazazi au ndugu wa karibu wanaoweza kumtembelea mwanafunzi awapo shuleni pamoja na namba zao za simu.
VI. Mwanafinzi anatakiwa kuonesha leaving certificate, Result slip , Bank pay in slip na vifaa vingine anavyotakiwa kuwasilisha anaporipoti ndipo atapokelewa na kusajiliwa na si vinginevyo. Hivyo ni muhimu kuja na vitu hivyo.

NB: Kumbuka kuwa wewe umebahatika kupata nafasi hii ya pekee kati ya maelfu ya wanafunzi waliofanya mtihani. Hivyo ni lazima kuitumia nafasi hii kwa faida yako na Taifa. Kinachokuleta katika shule hii ni kujifunza na kuelimika hivyo unatakiwa kudumisha heshima na sifa ya shule hii ya kyerwa modern, Unapofika ripoti kwa mwalimu wa zamu au ofsi ya malezi au makamu mkuu wa shule au mkuu wa shule ili upewe maelekezo zaidi.

SHULE YA SEKONDARI KYERWA MODERN

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE YA SEKONDARI KYERWA MODERN

Shule hii inaendeshwa kwa mjibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yemye dhamana ya Elimu nchini. Wewe kama mwanafunzi unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote , wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparations)
d) Kuwahi katika shughuli za shule na zingine utakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hivo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
g) Kuvaa sare ya shule wakati unaotakiwa
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
i) Kutomiliki na kutumia SIMU AU VIFAA VINAVYOHUSIANA NA SIMU (Mfano charger, line, betri ya simu n.k) katika mazingira ya shule.
j) Kupita njia sahihi utokapo na uingiapo katika eneo la shule kwa ruhusa (kibali) maalumu,

2. Makosa yanayoweza kusababisha ukafukuzwa shule baadhi ni kama yafuatayo:-

a) Wizi
b) Uasherati
c) Ubakaji na ushoga
d) Kusuka nywele kwa mtindo wowote usio ruhusiwa uwapo shuleni
e) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
f) Uvutaji bangi
g) Makosa ya jinai.
h) Kupiga au kupigana
i) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
j) Kudharau bendera ya Taifa
k) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
l) Kutoa mimba
m) Kugoma, kuchochea na kuongoza vurugu au kuvuruga amani na usalama wa shule na watu
n) Kukataa adhabu kwa makusudi
o) Utoro wa vipindi na kutohudhuria masomo kwa muda wa siku tisini (90) mfululizo bila taarifa rasmi, kutofanya mazoezi, majaribio na mitihani mbalimbali bila sababu maalum.
p) KUMILIKI NA KUTUMIA SIMU, laini chaja, na viashiria vinavyopelekea kuwa na simu katika mazingira ya shule.
q) Kupita njia zisizoruhusiwa kwa mujibu wa sheria wakati wa kutoka na kuingia katika eneo la shule na uwapo ndani ya shule kwa mfano KURUKA UKUTA/UZIO wa shule. KURUKA DIRISHA. N.k
r) Kuvaa mavazi yanayobana na milegezo

NI WAJIBU WA KILA MWANAFUNZI KUTII TARATIBU KANUNI NA SHERIA ZA SHULE BILA KUSHURUTISHWA

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

……………………………………

**JOSINA DEUS RUTAKYAMIRWA**

**MKUU WA SHULE**

KIAMBATISHO A

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A:
……………………………………
……………………………………
…………………………………….

To the medical officer
………………………………….
………………………………….

Date, ………………… From:

Re

------------------------------------------------------------------------------

Please Examine the above named as to his / her physical and mental fitness for a full-time secondary school studies. The examination should include the following categories (I-IV) each category or sub- allegory of which will render the applicant ineligible in case of defect. Pregnant category (category IV) will also render a girl candidate ineligible for the course.

a) Eye sight
b) Hearing
c) Speech
d) General disease
e) Leprosy
f) Epilepsy
g) Limbs

Other ………………………………………………………………….

Disease …………………………………………………………….      serious

Pregnancy

PART B: MEDICAL OFFICER:

(To be completed by a government medical officer)

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit for a full-time secondary school studies.

a) eye sight
b) Hearing
c) speech
d) (General disease)
e) Epilepsy

Neuroses ………………………………………………………………….

(Dier serious disease …………………………………………………

Pregnancy ……………………………………………………………

DATE ………………………………………. SIGNATURE …………………………….

STATION ……………………………………………………………………………….

……………………

**JOSINA DEUS RUTAKYAMIRWA**
**MKUU WA SHULE**

KIAMBATISHO B

SHULE YA SEKONDARI KYERWA MODERN

FOMU YA TAARIFA BINAFSI ZA MWWANAFUNZI.

SEHEMU A:

1. Jina kamili la mwanafunzi …………………………………………
2. Mwaka wa kuzaliwa ……………………… kabila ………………………..
3. Jina la mzazi/ mlezi …………………………………………………
4. Uhusiano …………………………..kazi yake ………………………..
5. Anuani ya mzazi / mlezi ……………………………………………
6. Namba ya simu ya mzazi/ mlezi ……………………………………….
7. Umbali kuja shuleni ni KM ……………………………………
8. Majina ya ndugu /walezi wengine wa karibu:-

| JINA | UHUSIANO | NAMBA YA SIMU | MAHALI ALIPO |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

9. MENGINEYO:

( Kama Mwanafunzi ni mgonjwa aje na uthibitisho wa daktari kama ni yatima aje na hati ya kifo kama ni mlemavu n.k)
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

SEHEMU B:

TAMKO LA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KYERWA MODERN

Mimi ………………………………………. (majina matatu) nimezisoma na kuzielewa sheria, kanuni na taratibu za shule na kwamba niko tayari/ siko tayari kuzifuata.

Sahihi ya mwanafunzi …………………… tarehe ………………………………..

SEHEMU C:

TAMKO / AHADI YA MZAZI / MLEZI

Mimi ………………………………………. Ambaye ni mzazi wa / mlezi wa mwanafunzi …………………………………ninaahidi nitatekeleza maagizo na mahitaji yote muhimu ya shule kama ilivyoelekezwa na kwamba niko tayari kushirikiana na viongozi wa shule katika suala zima la malezi na maadili mema ya mtoto wangu ili kuinua taaluma na nidhamu yake pia ninakubali kutii taratibu, kanuni na sheria zote za shule na kulipa

michango mingine kama ilivyoelekezwa pia nitafuata maelekezo mengine kadri yatakavyo tolewa na uongozi wa shule ya sekondari Kyerwa Modern

Sahihi ya mzazi / mlezi …………………………………. Tarehe ………………………

**<u>KIAPO CHA MWANAFUNZI</u>**

Mimi mwanafunzi wa shule ya Sekondari Kyerwa Modern. Nimekubali kuishi katika jumuiya hii nikiwa mtiifu na kufuata sheria za shule kwa mjibu wa sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 kama ilivyorekebishwa na sheria Na 10 ya mwaka 1995. Bodi ya shule imepewa mamlaka ya kusimamia nidhamu ya wanafunzi. Hivyo nina ahidi kutii utaratibu wote ulioainishwa kwenye sheria za shule wakati wote ninapokuwa mwanafunzi .

Hivyo mimi ………………………… (Majina matatu) nikiwa mwanafunzi wa kidato cha tano (5) katika shule ya Sekondari Kyerwa Modern ninaapa kutomiliki simu ama kifaa chochote kinachohusiana simu pamoja na urukaji ukuta (fance) wa shule pia kutoshiriki kuanzisha mgomo, fujo. Ninahaidi kuwa mtiifu na mwanafunzi mwenye adabu

Pia leo tarehe ……….. mwezi ……………… mwaka ……………. Ninahaidi kuwa nikikamatwa na simu ama kifaa kinachoashiria mimi kumiliki simu na nimeruka uzio/ukuta (fance) wa shule Pamoja na makosa mengine ambayo ni kinyume na taratibu, kanuni na sheria nifukuzwe shule kabisa.

……………………………………… (majina matatu) Leo tarehe ……………………….

Mimi

Sahihi

Mbele ya Mkuu wa shule ya Sekondari Kyerwa Modern kwa niaba ya bodi ya shule ya Sekondari Kyerwa Modern.

……………………………………

KATIBU WA BODI YA SHULE Muhuri wa ofisi

.

KIAMBATISHO C

SHULE YA SEKONDARI KYERWA MODERN

TAARIFA ZA NDUGU (WAZAZI / WALEZI) WA MWANAFUNZI WATAKAORUHUSIWA KUMTEMBELEA MWANAFUNZIAWAPO SHULENI

| | |
|---|---|
| JINA …………………………………… | JINA ………………………………… |
| UHUSIANO …………………………. | UHUSIANO ………………………… |
| ANAKOTOKA ……………………. | ANAKOTOKA ……………………… |
| ANUANI …………………… | ANUANI …………………………… |
| NAMBA YA SIMU ……………………… | NAMBA YA SIMU ………………… |
| PICHA | PICHA |

| | |
|---|---|
| JINA ………………………………. | JINA …………………………………. |
| UHUSIANO ……………………….. | UHUSIANO ………………………… |
| ANAKOTOKA …………………… | ANATOKA ………………………… |
| NAMBA YA SIMU ………………….. | NAMBA YA SIMU ………………… |
| PICHA | PICHA |

Mimi (mwanafunzi ) kidato cha …………………… kuanzia mwaka wa masomo ……………………hadi ……………………. Nathibitisha kuwa watu na wenye picha hapo juu ni wazazi/ walezi / ndugu zangu watakaonitembelea muda wote nitakapokuwa katika shule hii ya Kyerwa Modern Sekondari

Sahihi …………………………  Tarehe …………………………